

MFUMO WA TATHMINI WA TAARIFA (IRM):

TANZANIA TAARIFA YA MWISHO WA UTEKELEZAJI 2014–2016

Ngunga Greyson Tepani
Mtafiti wa IRM
Taarifa ya Mwishoni mwa Utekelezaji 2014-2016
First End-of-Term Report

Open
Government
Partnership

INDEPENDENT
REPORTING MECHANISM

INDEPENDENT REPORTING MECHANISM (IRM): TANZANIA END-OF-TERM REPORT 2014-2016

Tanzania's second action plan focused on improving public access to information in important sectors including land and extractives. The Access to Information Act was enacted shortly after the action plan ended, and it represents a major step forward for increasing government transparency. Although the commitments were ambitious and highly relevant to opening government, successful implementation was limited. Moving forward, the government could focus on improving institutional capacity to carry out commitments.

The Open Government Partnership (OGP) is a voluntary international initiative that aims to secure commitments from governments to their citizenry to promote transparency, empower citizens, fight corruption, and harness new technologies to strengthen governance.

The Independent Reporting Mechanism (IRM) carries out a review of the activities of each OGP participating country. This report is a summary of the results in implementing OGP commitments for Tanzania for the period July 2014 to June 2016. Additionally, some relevant developments that happened up to mid-September 2016 are also included.

The State House Good Governance Coordination Unit, located in the presidency, serves as the secretariat of OGP in Tanzania. Further support for implementation of commitments at the city, municipal, and district level comes from the Prime Minister's Office for Regional Administration and Local Government.

A Steering Committee, composed of government officials and civil society representatives, oversees the implementation of the second action plan. Consultations with stakeholders were done during the development of the second action plan (2014–2016) through face-to-face interactions and online submissions. The stakeholders consulted include local civil society organisations (CSOs) though only about four of these CSO groups were involved in the actual implementation of the country's action plan.

At the time of publishing this report, the commitment on enacting access to information legislation is complete, and the government made substantial progress on two other commitments since the latest IRM midterm report. The government published its end-of-term self-assessment report in March 2016. Tanzania has already drafted its third OGP action plan (2016–2018) with seven commitments in total, five of which have been carried forward. Two additional commitments have been added, focusing on medical and health services and performance management. Although the commitment on the Access to Information Act was completed, it has been carried forward from the previous action plan (2014–2016) with a focus on implementation. The first of the seven commitments is on enacting the Access to Information Act and its guidelines.¹

TABLE 1: AT A GLANCE

NUMBER OF COMMITMENTS: 5

NUMBER OF MILESTONES: 16

LEVEL OF COMPLETION

	MIDTERM	END OF TERM
COMPLETED:	0	0
SUBSTANTIAL:	0	2
LIMITED:	4	3
NOT STARTED:	1	0

NUMBER OF COMMITMENTS WITH:

CLEAR RELEVANCE TO OGP VALUES:	5	5
TRANSFORMATIVE POTENTIAL IMPACT	1	1
SUBSTANTIAL OR COMPLETE IMPLEMENTATION	0	2
ALL THREE (🌟):	0	1

DID IT OPEN GOVERNMENT?

MAJOR	N/A	2
OUTSTANDING	N/A	0

MOVING FORWARD

COMMITMENTS CARRIED OVER TO NEXT ACTION PLAN:	5
---	---

Table 2. Overview: Assessment of Progress by Commitment

COMMITMENT OVERVIEW	SPECIFICITY				OGP VALUE RELEVANCE <i>(as written)</i>				POTENTIAL IMPACT				COMPLETION		MIDTERM		DID IT OPEN GOVERNMENT?					
	None	Low	Medium	High	Access to Information	Civic participation	Public Accountability	Technology & Innovation for Transparency & Accountability	None	Minor	Moderate	Transformative	Not started	Limited	Substantial	Complete	Worsens	Did not change	Marginal	Major	Outstanding	
3.1. Access to Information				X	X						X			X							X	
3.2. Open Data			X		X		X			X			X		X						X	
3.3. Open Budgets				X	X		X	X		X			X	X						X		
3.4. Land Transparency			X		X		X			X			X	X						X		
3.5. Extractive Industry Transparency				X	X		X			X		X		X						X		

¹[http://www.twaweza.org/uploads/files/FINAL%20OGP%](http://www.twaweza.org/uploads/files/FINAL%20OGP%20Report%202014-2016.pdf)

MFUMO WA TATHMINI WA TAARIFA (IRM): TANZANIA TAARIFA YA MWISHO WA UTEKELEZAJI 2014-2016

Mpango kazi wa pili wa Tanzania ulilenga kuboresha upatikanaji wa taarifa kwa Wananchi kwa sekta muhimu zikiwemo ardhi na tasnia ya uziduaji. Sheria ya upatikanaji taarifa ilipitishwa mara baada ya muda wa utekelezaji mpango kazi kuisha, sheria hiyo ikiwakilisha hatua moja kubwa ya kukuza uwazi serikalini. Ingawa maazimio yalikuwa na utashi mkubwa na yenye umuhimu katika “kuifungua serikali”, utekelezaji wake ulikuwa hafifu. Tunaposonga mbele, serikali inaweza kujikita katika kuboresha uwezo wa kitaasisi kutekeleza maazimio.

Mpango wa Utendaji Kazi wa Serikali kwa Uwazi (OGP) ni juhudi za wadau kadhaa, wanaojitolea kimataifa kwa nia ya kupata maazimio mahususi kutoka katika serikali mbalimbali kwa wananchi wake yatakatimiza uwazi, kuwezesha wananchi, kupambana na rushwa na kutumia teknolojia mpya ili kuboresha utawala bora.

Mfumo wa Tathmini wa Taarifa (IRM) unahakiki shughuli za kila nchi inayoshiriki OGP. Taarifa hii ni muhtasari wa matokeo ya utekelezaji wa maazimio ya OGP nchini Tanzania kwa kipindi cha Julai 2014 hadi Juni 2016. Pia, taarifa inajumuisha baadhi ya hatua zilizofikiwa kiutekelezaji hadi kufikia katikati ya mwezi Septemba 2016.

Kitengo cha Uratibu wa Utawala Bora, kilichopo Ikulu ya Rais, ndio sekretarieti ya OGP nchini Tanzania. Pia, msaada wa utekelezaji wa maazimio hupatikana katika ngazi ya jiji, manisipaa na wilaya kupitia Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI).

Kamati Elekezi, inayoundwa na wawakilishi kutoka serikalini na asasi za kiraia husimamia utekelezaji wa mpango kazi wa pili (wa OGP). Wakati ikiandaa mpango kazi wa pili (2014–2016), serikali ilifanya mashauriano na wadau kupitia mikutano ya ana kwa ana na maoni mtandaoni. Wadau waliofikiwa na mashauriano hayo ni pamoja na asasi za kiraia (AzaKi) ingawa takribani ni AzaKi nne tu ndio zilizoshiriki kikamilifu katika utekelezaji wa mpango kazi huo.

Hadi taarifa hii ikichapishwa, azimio juu ya sheria ya upatikanaji taarifa lilikuwa limekamilika, na pia serikali ilipiga hatua kubwa katika utekelezaji wa maazimio mengine mawili tangu pale taarifa ya nusu-muhula ya IRM ilipotoka. Serikali ilichapisha taarifa yake ya kujitathmini kwa mwisho wa utekelezaji wa mpango kazi iliyotoka mnamo mwezi Machi 2016. Tanzania imeshaandaa rasimu ya mpango kazi wake wa tatu wa OGP (2016–2018) ukiwa na jumla ya maazimio saba, matano kati ya hayo yameridua kutoka mpango kazi uliopita. Maazimio mapya mawili yameongezwa, yakitazama zaidi juu ya huduma za madawa na afya; na usimamizi wa utendaji. Ingawa azimio juu ya sheria ya upatikanaji taarifa lilishatelezwa, limebakizwa toka mpango kazi uliopita (2014–2016) kwa kuzingatia utekelezaji wa sheria yenyewe. Azimio la kwanza kati ya saba ya mpango kazi mpya linahusu kuunda sheria ya upatikanaji taarifa na kanuni za utekelezaji wake.

JEDWALI 1: KWA UFUPI

IDADI YA MAAZIMIO: 5

IDADI YA HATUA: 16

KIWANGO CHA UTEKELEZAJI (MAAZIMIO)

	NUSU-MUHULA	MWISHONI
YALIYOKAMILIKA:	0	0
KWA KIASI KIKUBWA:	0	2
KIDOGO:	4	3
BADO KUANZA:	1	0

IDADI YA MAAZIMIO YENYE:

UHUSIANO WA WAZI NA TUNU ZA OGP:	5	5
ATHARI KUBWA ZA MABADILIKO	1	1
YALIYOKAMILIKA KWA KIASI KIKUBWA AU KUISHA KABISA	0	2
VIGEZO VYOTE VITATU (🗳️):	0	1

MAAZIMIO YALIYOIFUNGUA SERIKALI?

UFUNGUAJI MKUBWA	N/A	2
UFUNGUAJI ULIOJIPAMBANUA	N/A	0

MUENDELEZO

IDADI YA MAAZIMIO YALIYOSOGZWA KWENYE MPANGO KAZI UJAO:		5
---	--	---

USHIRIKI WA AZAKI WAKATI WA UTEKELEZAJI

Nchi zinazoshiriki mpango wa OGP hufuata mchakato wa kushirikisha wakati wa kuandaa mpango kazi na utekelezaji.

Tanzania ina Kamati Elekezi ya OGP, ambayo ni jukwaa la majadiliano, usimamizi, na ushauri juu ya upangaji na utekelezaji wa maazimio ya OGP. Kamati hiyo inaundwa na wawakilishi kutoka wizara, idara na wakala husika za serikali (MDAs) na asasi za kiraia (AzaKi) na kamati hukutana mara moja kila robo mwaka. Twaweza, *Tanganyika Law Society*, REPOA, na *Foundation for Civil Society* zilikuwa ni AzaKi zilizounda kamati elekezi ya OGP nchini. Kwa kipindi kilichofuata baada ya nusu-muhula, zaidi ya vikao viwili vya kamati elekezi vilifanyika ikiwa ni pamoja na kile cha kuandaa mpango kazi wa tatu. Vikao hivi vya kamati elekezi vilibaki kuwa jukwaa kwa waalikwa tu

Jedwali la 2: Mchakato wa Mashauriano wakati wa Kuandaa Mpango Kazi

AWAMU YA MPANGO KAZI	SHARTI LA MCHAKATO WA OGP (SEHEMU YA VIFUNGU VYA USIMAMIZI)	JE, SERIKALI ILITIMIZA SHARTI HILI?
Wakati wa Utekelezaji	Je, kulikuwepo na jukwaa la mara kwa mara la mashauriano wakati wa utekelezaji mpango?	Ndiyo
	Mashauriano: Yalikuwa wazi mtu yeyote kushiriki au kwa kualikwa tu?	Kwa kualikwa tu
	Mashauriano kwenye spektra ya IAP2 ¹	Shauriana

HATUA ILIYOFIKIWA KATIKA UTEKELEZAJI MAAZIMIO

Kama sehemu ya OGP, nchi zinazoshirika zinawajibika kuweka maazimio kwenye mpango kazi wa miaka miwili. Taarifa ya mwisho wa utekelezaji inatathmini kipimo / kigezo cha ziada, “je azimio liliifungua serikali?” Majedwali hapo chini yanaonyesha kwa muhtasari hatua ya utekelezaji iliyofikiwa mwishoni mwa utekelezaji mpango na uchambuzi wa kipimo / kigezo hiki. Katika mpango kazi wa pili wa OGP, Tanzania ilikuwa na maazimio matano na hatua 17 za kufikia maazimio hayo. IRM haikuona haja ya kuweka kongu za maazimio hayo sababu ya uchache. Azimio la kutunga sheria ya upatikanaji taarifa lilikamilika utendaji wake katika kipindi cha utekelezaji wa mpango kazi wa pili. Kuandaa kanuni ambazo ni muhimu kwa utekelezaji wa sheria tajwa ni sehemu ya azimio iliyoingizwa kwenye mpango kazi wa tatu wa OGP, zikitarajiwa kukamilika ifikapo Juni 2017.

Vipaumbele vya mpango kazi wa pili wa OGP vilikuwa juu ya upatikanaji taarifa, uwajibikaji kwa umma, na matumizi ya teknolojia kukuza uwajibikaji na uwazi katika utoaji wa huduma serikalini. Rasimu ya mpango kazi wa tatu wa OGP imezingatia uzoefu na mafundisho yaliyopatikana tokana na mpango kazi uliopita, ikiwa ni pamoja na maoni yenye kujenga kutoka kwa asasi za kiraia na MDAs; na mapendekezo yaliyotolewa na IRM. Maazimio yaliyomo kwenye mpango kazi wa tatu wa OGP yamelenga vipaumbele vya mageuzi ya uwazi serikalini kwa kuimarisha uwazi, uwajibikaji, na ushiriki wa wananchi. Jumla ya maazimio saba yanapendekezwa kwenye mpango kazi mpya wa OGP, matano kati yao ni kutoka katika mpango kazi uliopita. Maazimio mapya mawili yanahusu huduma za madawa na afya; na mifumo ya usimamizi wa utendaji.¹

Viashiria na methodolojia zilizotumika wakati wa tathmini ya IRM zinaweza kupatikana kwenye Mwongozo wa Kufanya Tathmini za IRM, unaopatikana katika tovuti hii <http://www.opengovpartnership.org/about/about-irm>.

¹ “IAP2 Spectrum of Political Participation,” International Association for Public Participation, http://c.y.mcdn.com/sites/www.iap2.org/resource/resmgr/Foundations_Course/IAP2_P2_Spectrum.pdf

Kipimo kimoja kina umuhimu wa pekee kwa wasomaji na kinasaidia kuongeza kasi baina ya nchi zinazoshiriki mpango wa OGP: “azimio nyota” (★). Maazimio nyota yanachukuliwa kuwa ni maazimio mfano kwa OGP. Ili kupata nyota, azimio lazima likidhi vigezo kadhaa:

1. Lazima liwe la kipekee sana ambapo uamuzi juu ya utashi tarajali wake unaweza kufanywa. Maazimio nyota yatakuwa na umahsusi wa “wastani” au “juu”.
2. Lugha iliyotumika kwenye azimio ni lazima ioneshe wazi uhusiano wake na “kuifungua serikali”. Lazima kuwe na uhusiano wa kipekee na angalau moja ya tunu za OGP (Upatikanaji wa taarifa, Ushiriki wa Wananchi au Uwajibikaji kwa Umma).
3. Azimio litaleta “athari kubwa” inayotarajiwa endapo litatekelezwa kikamilifu.
4. Mwisho, azimio ni lazima litekelezwe “kwa kiasi kikubwa” au “kwisha kabisa” kwa wakati uliopangwa kutekelezwa kwa mpango kazi.

Kwa kuzingatia vigezo hivi (ambavyo vilibadilika mnamo mwaka 2015), mpango kazi wa Tanzania haukuwa na maazimio nyota kwa kipindi cha nusu-muhula isipokuwa azimio moja (azimio 3.1) ilipofika mwishoni mwa utekelezaji mpango.

Maazimio yalitathminiwa kuwa ni nyota wakati wa kuandaa taarifa ya nusu-muhula yanaweza kupoteza hadhi hiyo endapo utekelezaji wake utakuwa chini ya kiwango cha kwa kiasi kikubwa au kuisha kabisa inapofika mwishoni mwa mzunguko wa utekelezaji wa mpango kazi wote. IRM inatathmini hatua iliyofikiwa ya utekelezaji ya azimio kwa muda wote wa mpango kazi.

Mwisho, grafu zilizomo kwenye sehemu hii zinaonyesha muhtasari tu wa utajiri wa takwimu zinazokusanywa na IRM wakati wa mchakato wa kuandaa taarifa ya utekelezaji. Kwa takwimu zote za Tanzania, na nchi nyingine zinazoshiriki mpango wa OGP, tazama OGP Explorer kwenye tovuti hii www.opengovpartnership.org/explorer.

KUHUSU “AZIMIO LILIFUNGUA SERIKALI?”

Mara nyingi, maazimio ya OGP yanakuwa na maneno yasiyo dhahiri au hayako wazi juu ya kuifungua serikali, lakini hufanikiwa kufanya mageuzi makubwa kisiasa. Mara nyingine, maazimio yaliyofikia hatua kubwa kiutekelezaji yanaweza kuonekana yenye umuhimu na utashi, lakini yakashindwa kuifungua serikali. Katika juhudi za kujumuisha hali hizo tata na, muhimu zaidi, mabadiliko halisi katika utendaji wa serikali, IRM ilitambulisha kigezo kipa—“je, azimio liliifungua serikali?”—katika taarifa za mwisho wa utekelezaji. Kigezo hiki kinajaribu kwenda mbali ziadi ya kutathmini kilichopatikana na matokeo hadi kuangalia namna utendaji serikalini ulivyobadilika kutokana na utekelezaji wa azimio. Hii ni tofauti na “maazimio nyota” ya IRM ambayo yanaelezea kiwango cha athari *tarajali*.

Watafiti wa IRM hutathmini swali la “je, azimio liliifungua serikali?” kwa kutazama kila tunu ya OGP inayohusika kwa azimio hilo. Tunauliza, “Je, azimio lilipanua wigo wa utendaji serikali mbali zaidi ya utendaji wake wa kawaida?” Mizania ya tathmini ni kama ifuatavyo:

- Iliharibika: Azimio linaharibu uwazi serikalini kutokana na hatua zilizochukuliwa wakati wa utekelezaji wa azimio.
- Haikubadilika: Azimio halikubadili hali ya utendaji serikalini.
- Kidogo: Kuna mabadiliko, lakini ni kiduchu kwa athari ya kukuza uwazi.
- Kubwa: Ni hatua moja ya uwazi serikalini katika eneo husika kisera, lakini bado wigo au ukubwa wake una ukomo.
- Imejipambanua: Mageuzi yaliyobadilisha “biashara kama kawaida” kwa eneo husika kisera kwa kuifungua serikali.

Ili kutathmini, watafiti huweka wazi hali ilivyokuwa kabla mpango kazi haujaanza kutekelezwa. Kisha hutathmini mabadiliko yoyote *kama yaliyofanyika* kwa kuangalia mabadiliko ya uwazi serikalini.

Wasomaji wetu ni budi wakatambua mipaka iliyopo. Taarifa za IRM za mwisho wa utekelezaji zinaandaliwa miezi kadhaa baada ya mzunguko wa muda wa mpango kazi kukamilika. Vigezo vinatazama matokeo yaliyoonekana katika uwazi wa utendaji serikalini inapofika mwishoni mwa kipindi cha utekelezaji cha miaka miwili. Taarifa hizi na vigezo hazina nia ya kupima athari sababu ya maana itakayoletwa na methodolojia ngumu na kipindi kinachoangaliwa na taarifa.

Jedwali la 3: Mapitio, tathmini ya hatua iliyofikiwa kwa kila azimio

MAPITIO YA AZIMIO	UMAHUSI				UHUSIANO NA TUNU ZA OGP (kama ilivyoandikwa)				ATHARI TARAJALI				UTEKELEZAJI		NUSU-MUHULA MWISHONI		JE, ILIIFUNGUA SERIKALI?				
	Hakuna	Mdogo	Wastani	Uko juu	Upatikanaji taarifa	Ushiriki wa wananchi	Uwajibikaji kwa umma	Teknolojia & Ubunifu kwa ajili ya Uwazi & Uwajibikaji	Hakuna	Ndogo	Wastani	Mabadiliko makubwa	Haujaanza	Kiasi kidogo	Kiasi kikubwa	Umekamilika	Iliharibika	Haikubadilika	Kiasi kidogo	Kiasi kikubwa	Imejipambanua
3.1. Upatikanaji Taarifa				X	X						X		X		X					X	
3.2. Takwimu Huria			X		X		X			X			X		X					X	
3.3. Uwazi katika Bajeti				X	X	X	X			X			X						X		
3.4. Uwazi katika sekta ya Ardhi			X		X		X			X			X						X		
3.5. Uwazi tasnia ya Uzidujaji				X	X	X				X		X							X		

¹http://www.twaweza.org/uploads/files/FINAL%20OGP%20ACTION%20PLAN%20III%2030_8_2016.pdf.

3.1 | SHERIA YA UPATIKANAJI TAARIFA

Maelezo kamili:

Kutunga Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa itakapofika Desemba mwaka 2014

Sheria itatungwa kwa kuzingatia mifano bora kimataifa na itajumuisha:

(i) Kutambua uwepo wa haki ya kupata taarifa, pamoja na matarajio mapana ya uwazi wa taarifa zinazoshikiliwa na taasisi za umma, na za binafsi zinazofanya kazi za uma au zinazofadhiliwa na fedha za umma;

(ii) Wajibu wa kuchapisha taarifa kwa upana zaidi na bila kushurutishwa/kuombwa;

(iii) Taratibu imara za kuandaa na kushughulikia maombi ambazo ni rahisi, bure na haraka (zikionyesha wazi muda wa kupata majibu/taarifa).

(iv) Orodha fupi ya taarifa zilizoruhusiwa zinazotokana na masuala ya ulinzi na usalama, maslahi ya umma yanaposhika hatamu na kukataliwa pale ambapo sehemu ya taarifa imeruhusiwa;

(v) Haki ya kukata rufaa.

(vi) Ulinzi kwa kutoa taarifa za nia njema na adhabu kwa kuzuia upatikanaji wa taarifa; na

(vii) Wajibu wa kutoa taarifa juu ya maombi yaliyopokelewa na kuhakikisha kuna adhabu zinatolewa kwa kukataa kutoa taarifa bila ya sababu za msingi.

Taasisi kiongozi: Wizara ya Katiba na Sheria (MoCLA)

Taasisi saidizi: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu (AG), AzaKi na asasi za sekta binafsi ambazo hazikutajwa

Tarehe ya kuanza: 1 Julai 2014

Tarehe ya mwisho: 31 Desemba 2014

MAPITIO YA AZIMIO	UMAHSUSI				UHUSIANO NA TUNU ZA OGP (kama ilivyoandikwa)				ATHARI TARAJALI				UTEKELEZAJI		NUSU-MUHULA MWISHONI		JE, ILIIFUNGUA SERIKALI?				
	Hakuna	Mdogo	Wastani	Uko juu	Upatikanaji taarifa	Ushiriki wa wananchi	Uwajibikaji kwa umma	Teknolojia & Ubunifu kwa ajili ya Uwazi & Uwajibikaji	Hakuna	Ndogo	Wastani	Mabadiliko makubwa	Haujaanza	Kiasi kidogo	Kiasi kikubwa	Umekamilika	Iliharibika	Haikubadilika	Kiasi kidogo	Kiasi kikubwa	Imejipambanua
3.1. Kwa ujumla				X	X						X		X		X					X	

Maoni ya Mhariri: Azimio hili lina uhusiano na tunu za OGP kama lilivyoandikwa, linaweza kuleta athari za mabadiliko makubwa, na limetekelezwa kwa kiasi kikubwa au kumalizika na kwahiyoyo linakidhi kuwa azimio nyota.

LENGO LA AZIMIO

Azimio limekusudia kutungwa kwa sheria ya Upatinakanaji Taarifa (ATI), na ilitokana na azimio lililotangulia ambalo halikutekelezwa kwenye mpango kazi wa kwanza wa OGP nchini Tanzania (2012–2013). Mpango kazi wa kwanza wa OGP nchini Tanzania haukuwa na maelezo ya kina ya namna ya kuipata sheria hiyo. Hivyo basi serikali iliandaa azimio hili ili kuendana na mapendekezo ya taarifa ya tathmini ya IRM kwa mpango huo wa kwanza, na kuhusisha pia mashauriano na wadau na tarehe ya mwisho ya kupatikana kwa sheria.

Kabla ya uandaaji wa azimio hili kwenye mpango kazi wa pili wa OGP, upatikanaji wa taarifa zinazoshikiliwa na serikali ilikuwa vigumu, na hakukuwa na sharti lolote kisheria lililoilazimisha serikali kutoa taarifa.¹ Mara kwa mara masuala muhimu kwa jamii hayakuwekwa wazi, na watumishi wa serikali waliokuwa na dhamana ya kutoa taarifa hizo mara nyingi waliweka vikwazo kwa watumiaji au wale waliobahatika kupewa taarifa hizo. Hivyo basi azimio hili lina lengo la kuhakikisha taarifa zote zilizo mikononi mwa serikali zinapatikana kwa kila mtu, zikitolewa bila kupitisha muda uliopangwa, na kusambazwa miongoni mwa jamii, vyombo vya habari na Wananchi kwa ujumla.

HALI ILIVYO

Nusu-muhula: Kiasi kidogo

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2015, wizara ya Katiba na Sheria (MoCLA) ilikuwa imepiga hatua kidogo katika utekelezaji wa azimio hili. Ingawa muswada wa Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa ulisomwa kwa mara ya kwanza na ya pili, haukupitishwa na Bunge mnamo mwaka 2015. Bunge liliutupilia mbali muswada tajwa kwani haukuwa umeshirikisha wadau vya kutosha,² hili likaurudisha nyuma mchakato.³ Kwa mujibu wa wadau wa asasi za kiraia waliohojiwa, mchakato ulizidi kudorora pia kwa sababu za uchaguzi mkuu uliofbnyika tarehe 25 Oktoba 2015.

Ili kuupitisha muswada huo wa sheria, wizara ilibidi wauandae upya, kufanya mashauriano kwa mapana na wadau, na upitishwe na Bunge. Kwa maelezo ziaidi tafadhali soma Taarifa ya IRM ya nusu-muhula (2014–2016).

Mwishoni: Kiasi kikubwa

Azimio la kutunga sheria ya upatikanaji wa taarifa lilikamilika katika kipindi cha taarifa ya IRM ya mwisho wa kipindi cha mpango kazi lakini nje ya tarehe ya mwisho wa utekelezaji azimo ambayo ilikuwa ni tarehe 30 Juni 2016. Muswada ulipelekwa bungeni na kusomwa mara mbili, kujadiliwa, na hatimaye kupitishwa tarehe 6 Septemba 2016.

JE, AZIMIO LILIFUNGUA SERIKALI?

Upatikanaji taarifa: Kiasi kikubwa

Kutokana na kuwepo kwa sheria ya upatikanaji taarifa, raia wa Tanzania sasa wana haki kisheria kudai na kupata taarifa zinazoshikiliwa na serikali. Huko nyuma, mtu asingeweza kutaja kifungu chochote kisheria ili kupata taarifa kama hizo, labda tu kama angetaja Kifungu cha 18 cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano (URT, 1977). Sheria mpya ya upatikanaji taarifa inaongeza wingi wa taarifa zitakazokuwa rahisi kufikiwa na Wananchi, ingawa, sheria ina kifungu kidogo kinachokataza baadhi ya taarifa zisitolewe kifungu ambacho kinaweza kuzuia utoaji taarifa kwa ukamilifu.⁴

Mnamo Aprili 2015, Kituo cha Sheria na Demokrasia kilitoa alama 91 kati ya alama 150 kwa sheria iliyopitishwa kwa vile sheria ilihakikisha kunakuwa na haki ya kupata taarifa. Kituo kilisifu wigo mpana wa taarifa zitakazopatikana, ufinyu wa makatazo, na uwepo wa uangalizi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kama hatua muhimu zenye muelekeo chanya. Hata hivyo, Kituo hicho kilielezea masikitiko yake kwavile sheria ilikosa maelezo ya kina ya namna ya kukata rufaa endapo serikali ingeenda kinyume, kiasi kidogo cha hatua za kuhakikisha kunakuwa na weledi wa kutosha wa sheria, na kutoruhusu vyombo vya kisheria na watu wasio raia kutoruhusiwa na sheria.⁵ Mapengo haya bado yapo kwenye sheria iliyopitishwa na Bunge mwezi Septemba 2016.

Sheria ya upatikanaji taarifa ilipitishwa wakati ambapo serikali ilikuwa imeshafanya mabadiliko kadhaa kisheria ambayo yanaweza kuwa kikwazo kwa utekeleza timilifu wa sheria kwa kushindwa kuitumia ipasavyo haki ya kupata taarifa inayotolewa na sheria tajwa.⁶ Mtaalamu wa masuala ya upatikanaji taarifa kutoka mojawapo ya AzaKi nchini Tanzania⁷

alionyeshwa mashaka kuwa sheria haiendi mbali katika kuziba matundu ya kuingia taarifa ambazo serikali inaweza kuziita nyeti au takwimu ambazo zinaweza kuchukuliwa kuwa haziiipendezi serikali au zenye utata endapo zitatolewa kwa umma. Kwa mfano, sheria inaipa serikali siku 30 kujibu maombi ya kutaka taarifa, ambapo kwa mujibu wa Deodatus Balile, Makamu Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania ni muda mrefu sana kwa muandishi wa habari kusubiri.⁸

Wakati ambapo sheria ya upatikanaji wa taarifa ni kielelezo cha hatua muhimu iliyopigwa katika upatinakaji wa taarifa kisheria nchini Tanzania, bado haiko wazi ni kwa kiasi gani sheria hasi na kandamizi ya Makosa ya Kimtandao iliyopitishwa mwaka 2015 itaithiri sheria hii. Katika taarifa iliyoandaliwa na Privacy International, Ushirikiano Kimataifa wa Sera za TEHAMA kwa nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika (CIPESA), na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRD),⁹ vifungu 31, 32, 33, 34, 35, na 37 kwenye sheria ya Makosa ya Kimtandao¹⁰ “vinawapa mamlaka vyombo vya dola kupekua na kutwaa mifumo ya kompyuta, takwimu na taarifa bila ya hati ya mahakama na hivyo kuweza kuingilia haki ya kutobughudhiwa” na uhuru wa kupata taarifa.¹¹ Hali hii ya kukinzana kisheria kwa ufikiaji na matumizi ya taarifa kunaweza kuwafanya raia washindwe kutumia taarifa kwa uhuru ikiwemo matumizi ya asasi za kiraia.

Azimo hili linaonyesha mafanikio makubwa katika kuweka mifumo ya kisheria ya haki ya kupata taarifa. Wadau¹² wamesifu utungwaji wa sheria hii kuwa utafungua milango zaidi, hususan kwa vyombo vya uangalizi na wadau wengine kama vile AzaKi. Sheria hii inaweza kuwa muhimu kwa raia waliokuwa wakitaka kupata taarifa ambazo awali hazikupatikana juu ya sera na programu ambazo zinaathiri jamii zao moja kwa moja. Kwa mfano, Wananchi sasa wanaweza kutaka taarifa za bajeti na matumizi toka halmashauri wakiwa wanapima au kufuatilia mtiririko wa fedha (PETs) na shughuli zingine za kufuatilia uwajibikaji kwa jamii. Kuiweka haki ya kupata taarifa kisheria kunasaidia kuweka mazingira wezeshi ya kuwawajibisha watumishi wa umma.

KIPI KILICHOSOGZWA MBELE?

Rasimu ya mpango kazi wa tatu wa OGP¹³ inajumuisha na kutazama utekelezaji wa azimio hili ulipofikia, kwa kuwa na hatua mbili chini ya azimio jipya linalotaka kuundwa kwa sheria ya Upatikanaji Taarifa hadi kufikia mwezi Desemba 2016. Pendekezo jingine chini ya azimio jipya ni uandaaji wa kanuni za utekelezaji wa sheria ya Upatikanaji Taarifa hadi itakapofikia mwezi Juni 2017 kwa kushauriana na asasi za kiraia na wadau wengine. Rasimu ya mpango kazi huo inapatikana mtandaoni.¹⁴

Haijajulikana bado endapo azimio hili—kama lilivyoandikwa kwenye rasimu ya mpango kazi—litabakizwa ikizingatiwa kuwa tayari Bunge lishapitisha sheria tajwa kabla mpango kazi wa tatu wa OGP kukamilika. Wakati wa warsha ya mashauriano mnamo mwezi Septemba 2016 kupitia rasimu ya mpango kazi, wadau wa asasi za kiraia walidhani ya kuwa azimio hili lingeweza kuondolewa kabisa sababu ya hali halisi ya utekelezaji wake. Wengine walitoa sababu kuwa ni vyema kuwa na maazimio machache kwenye nyaraka ya mwisho ya mpango kazi. Waliona¹⁵ kuwa azimio hili lisiwemo kwenye mpango kazi ujao kwani hatua muhimu ya azimio hili (kuwepo kwa sheria) tayari imeshafikiwa kabla ya kuanza kwa utekelezaji wa mpango wa tatu wa OGP (Julai 2016–Juni 2018). Badala yake wanapendekeza azimio jipya liingizwe kuhusiana na kutangaza mali na madeni kwa wanasiasa viongozi na watumishi wa umma.

¹Lillian Nalwoga, “Access to Information in Tanzania: Laws, Policies, and Practice,” Collaboration on International ICT Policy in East and Southern Africa (CIPESA), 24 March 2015, <http://cipesa.org/2015/03/access-to-information-in-tanzania-laws-policies-and-practice/>.

²IRM Progress Report 2014–2016: Tanzania, http://www.opengovpartnership.org/sites/default/files/Tanzania_IRM_Progress_Report_2014-15_for_public_comment.pdf.

³Tanzania’s Parliament Rejects Media Censorship Bill, 21 November 2013, <http://bit.ly/1VIUcG9>.

⁴Mahojiano na mdau wa vyombo vya habari, 29 Septemba 2016, Dar es Salaam.

⁵Centre for Law and Democracy, Tanzania: Note on the Draft Access to Information Act, 2015, May 2015, <http://www.law-democracy.org/live/wp-content/uploads/2015/05/ATI-Law-analysis.rev.pdf>.

⁶Tanzania Assembly Backs Information Access Bill, FreedomInfo.org, 8 September 2016, <http://www.freedominfo.org/2016/09/tanzanian-assembly-hears-criticisms-of-pending-ati-bill/>.

⁷Mahojiano na mtaalamu ATI kutoka AZaKi, 21 Oktoba 2016, Dar es Salaam.

⁸<http://www.freedominfo.org/2016/09/tanzanian-assembly-hears-criticisms-of-pending-ati-bill/>.

⁹Muhtasari toka https://www.privacyinternational.org/sites/default/files/privacy_tanzania.pdf.

¹⁰Ibid.

¹¹Muhtasari toka https://www.privacyinternational.org/sites/default/files/privacy_tanzania.pdf.

¹²Mahojiano na chanzo ambacho hakikutaka kutajwa, 29 Septemba 2016, Dar es Salaam.

¹³Warsha ya wadau-mbalimbali kupitia rasimu ya mpango kazi wa tatu wa OGP Tanzania, iliyofanyika Ikulu Dar es Salaam, tarehe 6 Septemba 2016.

¹⁴http://www.twaweza.org/uploads/files/FINAL%20OGP%20ACTION%20PLAN%20II%2030_8_2016.pdf.

¹⁵Mahojiano na chanzo ambacho hakikutaka kutajwa, 24 Septemba 2016, Dar es Salaam.

3.2 | TAKWIMU HURIA

Maelezo kamili ya azimio:

Kuwa na mfumo wa takwimu huria hadi itakapofika Desemba 2016.

Hatua muhimu za utekelezaji wa azimio hili ni pamoja na zifuatazo:

(i) Kuanzisha chombo cha usimamizi au kikundi kazi chini ya Wizara ya Fedha ili kulitazama suala hili.

(ii) Miongozo itolewe, ikifuatiwa na maazimio ya kisheria yanayohimiza uwazi katika shughuli hizo na kuingiza dhana ya takwimu huria katika tafakuri za kiseru, ikiwa ni pamoja na utoaji wa takwimu zinazoweza kusomwa na kompyuta/mashine nyingine.

(iii) Uanzishwaji wa tovuti kuu ya takwimu ambayo ni rahisi kuitumia, na shirikishi yaani data.go.tz.

(iv) Uchapishaji wa seti muhimu za takwimu katika data.go.tz, hususan sekta za elimu, afya na maji, ikiwa ni pamoja na takwimu za Basic Education Statistics in Tanzania (BEST) na mitihani ya taifa (NECTA), vituo vya madawa na Bohari Kuu ya Madawa (MSD), vituo vya maji, usajili wa kampuni, takwimu kuhusu sensa na utafiti na takwimu za kitaalamu zinazooneshwa mipaka ya vijiji na kata; na kwa takwimu zote msisitizo uwekwe kwenye kutenganisha takwimu hadi kufikia ngazi ya vituo ili ziwe na manufaa kwa wananchi..

Shughuli za ziada kama zilivyoorodheshwa kwenye mpango wa utekelezaji:

- Kupitia upya sera, sheria na kanuni za utoaji wa takwimu/data.
- Kutunga sera ya takwimu huria.

Maoni ya uhariri: Hatua zilizohakikiwa katika azimio hili ni mchanganyiko wa hatua muhimu zilizomo ndani ya azimio lenyewe na shughuli zilizoelezwa katika mpango kazi

Taasisi kiongozi: Wizara ya Fedha (MoF), Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma (POPSM), Wakala wa Mitandao ya Serikali (eGA), Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (MoEVT), Wizara ya Maji (MoW), Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (MoHSW) na Ofisi ya Makumbusho ya Taifa.

Taasisi saidizi: Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), AzaKi na asasi za sekta binafsi ambazo hazikutajwa

Tarehe ya kuanza: Haikutajwa

Tarehe ya mwisho: 31 Desemba 2016

MAPITIO YA AZIMIO	UMAHSUSI				UHUSIANO NA TUNU ZA OGP (kama ilivyoandikwa)				ATHARI TARAJALI				UTEKELEZAJI		NUSU-MUHULA MWISHONI		JE, ILIIFUNGUA SERIKALI?				
	Hakuna	Mdogo	Wastani	Uko juu	Upatikanaji taarifa	Ushiriki wa wananchi	Uwajibikaji kwa umma	Teknolojia & Ubunifu kwa ajili ya Uwazi & Uwajibikaji	Hakuna	Ndogo	Wastani	Mabadiliko makubwa	Haujaanza	Kiasi kidogo	Kiasi kikubwa	Umekamilika	Iliharibika	Haikubadilika	Kiasi kidogo	Kiasi kikubwa	Imejipambanua
3.2. Kwa ujumla			X		X			X			X			X						X	

LENGO LA AZIMIO

Azimio hili limelenga kuunda mkakati wa takwimu huria nchini Tanzania ambao unajumuisha miongozo na sera, uanzishwaji wa chombo cha uangalizi, na kuruhusu wizara, idara na wakala za serikali (MDAs) kuchapisha takwimu haraka iwezekanavyo katika tovuti kuu ya takwimu huria.

Kabla ya utekelezaji wa azimio hili, takwimu kwa ujumla hazikuwa zikifikwa na umma. Kawaida ilikuwa kwamba taasisi za serikali zilizokuwa zikiongoza kwenye eneo fulani kila sera zilitoa na kuchapisha taarifa ndani ya taasisi, huku zikifichwa kuonekana kwa umma. Kwa zaidi ya miongo mine, takwimu zilizokuwa zikishikiliwa na serikali kama vile vyanzo vya maji, upatikanaji madawa, na takwimu za msingi za elimu zilibaki kuwa siri ya watendaji wachache serikalini, baadhi ya wajumbe wa kamati za bunge, na wabia wa maendeleo.

Azimio hili linaweka njia wazi ya kufungua takwimu za serikali na kuwawezesha Watanzania na umma kwa ujumla kufikia taarifa ambazo zinaweza kutumika tena. Kupitia utekelezaji wa azimio hili, serikali inaweza kujenga uaminifu wake kwa umma kwa kuwajibika au kuweka ushahidi wa huduma zilizotolewa.

HALI ILIVYO

Nusu-muhula: Kiasi kidogo

Mtafiti wa IRM aliona kuwa utekelezaji wa azimio hili lifanyika kwa kiasi kidogo. Tovuti kuu ya takwimu huria (www.opendata.go.tz) ilianzishwa na seti muhimu za takwimu zilichapishwa. Mtafiti huyo pia aligundua ya kuwa takwimu zilizochapishwa ziliweza kutafutwa kirahisi na kuwa mfumo wa takwimu zilizotumika kwenye tovuti kuu —*comma-separated-values* (CSV)—unaruhusu mafaili kufanyiwa kazi na watumiaji.¹ Hata hivyo, hatua zingine nne, ikiwa ni pamoja na uundwaji wa chombo cha uratibu chini ya uongozi wa Wizara ya Fedha, kupitia upya taratibu za utoaji takwimu huria, utoaji wa miongozo ya msaada kwa takwimu huria, na uandaaji wa sera ya takwimu huria, zilifanyika kwa kiasi kidogo au kutofanyika kabisa.

Ni muhimu kutambua ya kuwa wakati wa mpango kazi wa kwanza (2012–2013), serikali iliunda jukwaa la kuchapisha seti kadhaa za takwimu katika mfumo unaosomeka na kompyuta/mashine, ikiwa ni pamoja na seti za takwimu za utambuzi wa vyanzo vya maji.² Kwa mujibu wa mpango kazi wa sasa, tovuti kuu ilikuwa ijazwe na seti za takwimu kutoka sekta tatu: elimu, afya, na maji.

Taarifa ya nusu-muhula ya IRM ilipendekeza kuwa taasisi moja ya serikali iwe kiongozi wa kuratibu takwimu ili kuboresha ufanisi wa kuchapisha taarifa kwenye tovuti kuu kwa wakati. Mapendekezo mengine yalihuusu kuipitia upya sera ya utoaji takwimu huria, kuchapisha seti nyingi zaidi za takwimu huria kwenye tovuti kuu, kuandaa sera mpya ya takwimu huria, na kuunda chombo cha kusimamia michakato yote.³

Mwishoni: Kiasi kikubwa

Hadi kufikia Agosti 2016, jumla ya seti za takwimu 100 zilikuwa zimeshawekwa kwenye tovuti kuu (www.opendata.go.tz): 65 za elimu, 11 za maji, 10 za afya, na 14 zikitoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS).⁴ Mahojiano na wadau⁵ na taarifa ya kujitathmini ya serikali vinaonyesha kuwa sera ya takwimu huria bado inaandaliwa, na mapitio ya mwongozo wa utoaji wa takwimu huria yanafanyika.

Serikali pia ilitoa waraka wa takwimu huria mnamo mwezi Machi 2016 (URT, 2016) ikionyesha uwepo wa chombo cha kuratibu ukusanyaji, utayarishaji, na uchapishaji wa takwimu huria kwa MDA na serikali za mitaa. Ili kukamilisha utekelezaji wa azimio, uchapishaji wa seti zaidi za takwimu huria kwenye tovuti kuu katika mfumo unaosomeka na kompyuta/mashine unahitajika. Pia, sera mpya ya takwimu huria lazima iandaliwe. Wadau wa asasi za kiraia waliohojiwa⁶ wamehoji ufikiwaji na thamani ya takwimu zilizochapishwa kutokana na upenyaji hafifu wa intaneti nchini Tanzania. Wanaonelea kuwa takwimu hizo, au muhtasari wa waliyomo, zipatikane nje ya mtandao kwa Kiswahili na lugha nyepesi kuelewa na zipatikane kwa watu wengi zaidi nchini Tanzania.

Zaidi, rasimu ya tatu ya mpango kazi wa OGP (2016/17–2017/18) inatarajia kurekebisha tovuti kuu ya takwimu huria na kuiongezea seti nyingine za takwimu kwa kuzingatia maboresho mapya kiseru.⁷

JE, AZIMIO LILIFUNGUA SERIKALI?

Upatikanaji taarifa: Kiasi kikubwa

Azimio hili linalenga kuweka muundo wa takwimu huria ili umma uweze kufikia taarifa za serikali zenye ubora. Hata hivyo, pamoja na manufaa yanayotarajiwa, kuna sababu kadhaa zinakwamisha thamani ya azimio hili katika kuifungua serikali kupitia miradi mbalimbali ya takwimu huria, kama vile ukosefu wa upatikanaji wa intaneti kwa jamii kwa ujumla.⁸

Asasi ya *Tanzania Citizens Information Bureau* (TIB), AzaKi ambayo inashughulika na upatikanaji taarifa na masuala yanayoendana, imethibitisha kuwa seti za takwimu zilizochapishwa zimebadili namna Wananchi wanavyochukulia utendaji kazi wa serikali na kuweza kurudisha sehemu ya imani iliyokuwa imepotea.⁹ Tovuti kuu ina takwimu muhimu kwa jamii nchini Tanzania, takwimu kama zile zinazoonyesha uwiano wa wanafunzi kwa mwalimu mashuleni, vyanzo vya maji na ramani zake, na idadi ya wafanyakazi wa afya kwa kila mkoa. Takwimu hizi ambazo mwanzoni hazikupatikana kirahisi zinahusu sekta za afya, maji, na elimu na kwa mfumo wa mafaili yanayoweza kutumika tena ya aina ya CSV.¹⁰ Wakati ambapo taarifa inayopatikana ni muhimu sana kwa Wananchi, kiwango hafifu cha upenyaji wa intaneti (asilimia 4.9 kwa mwaka 2014) imekwamisha uwezo wa Wananchi kutumia tovuti kuu hiyo moja kwa moja.¹¹ Kwa mujibu wa ripoti ya *GovLab* ya mwaka 2016, wakati ambapo Wananchi wengi hawana uwezo wa kuwa na intaneti ili kuifikia tovuti kuu hiyo, asasi za kiraia zinaweza kutumika kama “wakala wa taarifa” na kufikisha taarifa kutoka kwenye tovuti kuu kwa njia nje ya mtandao kufikisha kwenye maeneo ambayo hayafikiwa na mtandao.¹²

Hatua nyingine za kuhakikisha kunakuwa na mrejesho toka kwa watumiaji ni kuunganisha tovuti kuu na teknolojia ya matumizi ya simu za mkononi. Hii ni muhimu hususan kwa sababu kumekuwa na ongezeko la matumizi ya simu za mkononi nchini Tanzania,¹³ na kuruhusu mrejesho wa Wananchi kupitia simu za mkononi kutaongeza uwezo wa Wananchi kushawishi na kudai utolewaji/uchapishwaji wa seti za takwimu. Zaidi, mtafiti wa IRM alibaini kutoka kwa afisa wa serikali¹⁴ kuwa mojawapo ya changamoto za kutumia takwimu ni kutokuwepo kwa teknolojia itakayorahisisha watumiaji nchini Tanzania kuzielewa na kuzifikia takwimu huria.

KIPI KILICHOSOGZWA MBELE?

Mpango kazi wa tatu wa OGP wa Tanzania una azimio kuhusiana na takwimu huria ambapo kipaumbele kimewekwa kwenye kukamilisha utekelezaji wa azimio hili. Zaidi ya hayo, kuna wazo la kuiboresha tovuti kuu kwa kuijenga upya na kuweka viwezeshi vitakavyoruhusu watumiaji kuleta mrejesho na fursa zaidi kuwasiliana na serikali mtandaoni kudai takwimu huria zilizo safi¹⁵.

¹The Open Data Institute, <http://bit.ly/1PSbMmA>.

²Ngunga Tepani, Tanzania OGP IRM Report. March 2014.

³Ngunga Tepani, Tanzania OGP IRM Report, December 2015.

⁴Mahojiano na afisa wa serikali ambaye hakutaka kutajwa, 24 Agosti 2016, Dar es Salaam.

⁵Mahojiano na afisa wa serikali ambaye hakutaka kutajwa, 23 Agosti 2016, Dar es Salaam.

⁶Mahojiano na mtaalamu wa ATI kutoka AzaKi, 21 Oktoba 2016, Dar es Salaam.

⁷http://www.twaweza.org/uploads/files/FINAL%20OGP%20ACTION%20PLAN%20III%2030_8_2016.pdf.

⁸<http://www.tcra.go.tz/images/documents/telecommunication/CommStatMarch16.pdf>.

⁹Mahojiano kwa njia ya simu na mdau wa asasi za kiraia, 13 Oktoba 2016, Dar es Salaam.

¹⁰<http://www.opendata.go.tz/dataset?organization=ministry-of-health-and-social>.

¹¹Juliet McMurren, David Sangokoya, Stefaan Verhulst, and Andrew Young, “Open Education Information in Tanzania: A Tale of Two Dashboards,” *GovLab*, 16 January 2016.

¹²<http://odimpact.org/case-open-education-information-in-tanzania.html>.

¹³*Ibid.*

¹⁴Subscription to Mobile and Fixed Network, April to June 2016, TCRA. Inapatikana <https://www.tcra.go.tz/images/documents/telecommunication/CommStatJune16.pdf>.

¹⁵Mahojiano na afisa wa serikali ambaye hakutaka kutajwa, 24 August 2016, Dar es Salaam.

¹⁶http://www.twaweza.org/uploads/files/FINAL%20OGP%20ACTION%20PLAN%20III%2030_8_2016.pdf

3.3 | UWAZI KATIKA BAJETI

Maelezo kamili ya azimio:

Kuwezesha upatikanaji wa takwimu za bajeti (taarifa muhimu nane) kwa umma , taarifa za ukaguzi za kamati za bunge na misamaha ya kodi hadi itakapofika Desemba 2014.

Kulingana na mifano bora ya kimataifa ya uwazi katika bajeti, hii itajumuisha:

(i) Kuchapisha, kwa wakati muafaka, taarifa muhimu za bajeti zifuatazo: taarifa kabla ya bajeti; muhtsari wa mapendekezo ya bajeti; bajeti iliyopitishwa; bajeti ya wananchi; taarifa za kila mwaka juu ya mapato yaliyokusanywa, matumizi na madeni; mapitio ya nusu-mwaka; taarifa ya mwisho wa mwaka; na taarifa za wakaguzi.

(ii) Kuchapisha taarifa za Kamati za Ukaguzi za Bunge.

(iii) Kuchapisha misamaha ya kodi, kila mwezi.

(iv) Kuchapisha takwimu kuhusu bajeti mtandaoni, katika mfumo unaowezesha kusomwa na kompyuta/mashine pia taarifa muhimu zipatikane katika halmashauri za wilaya na katika ngazi ya chini kabisa kama vile vituo vinavyotoa huduma ya elimu na afya.

Taasisi kiongozi: Wizara ya Fedha (MoF), Bunge, na ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG)

Taasisi saidizi: Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), AzaKi na asasi za sekta binafsi ambazo hazikutajwa

Tarehe ya kuanza: 1 Julai 2014

Tarehe ya mwisho: 30 Juni 2016

MAPITIO YA AZIMIO	UMAHSUSI				UHUSIANO NA TUNU ZA OGP (kama ilivyoandikwa)				ATHARI TARAJALI				UTEKELEZAJI		NUSU-MUHULA MWISHONI		JE, ILIIFUNGUA SERIKALI?				
	Hakuna	Mdogo	Wastani	Uko juu	Upatikanaji taarifa	Ushiriki wa wananchi	Uwajibikaji kwa umma	Teknolojia & Ubunifu kwa ajili ya Uwazi & Uwajibikaji	Hakuna	Ndogo	Wastani	Mabadiliko makubwa	Haujaanza	Kiasi kidogo	Kiasi kikubwa	Umekamilika	Iliharibika	Haikubadilika	Kiasi kidogo	Kiasi kikubwa	Imejipambanua
3.3. Kwa ujumla				X	X	X	X			X			X						X		

LENGO LA AZIMIO:

Azimio hili linaweka utashi mkubwa wa kuchapisha taarifa katika maeneo makuu matatu: bajeti, misamaha ya kodi, na kamati za ukaguzi za bunge.

Juhudi za kuziweka wazi taarifa kuu nane za bajeti kwa kuzingatia vigezo vya kimataifa vya uwazi katika bajeti na mifumo ya takwimu huria zilianza kabla ya azimio hili kuwepo. Tanzania imekuwa ikiweka wazi sita kati ya nyaraka hizo nane za bajeti kama zilivyoielezwa kwa kina kwenye azimio tangu mwaka 2012.¹ Taarifa hizo nane ni pamoja na (1) taarifa kabla ya bajeti; (2) muhtsari wa mapendekezo ya bajeti; (3) bajeti iliyopitishwa; (4) bajeti ya wananchi; (5) taarifa za kila mwaka juu ya mapato yaliyokusanywa, matumizi na madeni; (6) mapitio ya nusu-mwaka; (7) taarifa ya mwisho wa mwaka; na (8) taarifa za wakaguzi.

Pamoja na kuchapisha takwimu za bajeti mtandaoni kwa mfumo unaowezesha kusomwa na kompyuta/mashine, serikali pia iliahidi kupatikana kwa takwimu za bajeti nje ya mtandao katika ngazi ya halmashauri, ikiwa ni pamoja na mashuleni na vituo vya afya. Pia serikali iliahidi kuchapisha misamaha ya kodi na taarifa za kamati za ukaguzi za bunge kwa mara ya kwanza.

HALI ILIVYO

Nusu-muhula: Kiasi kidogo

Hadi kufikia katikati ya muhula wa utekelezaji azimio, ingawa kulikuwa na maboresho ya namna taarifa za bajeti zilivyokuwa zikitolewa, taarifa kuu mbili kati ya nane hazikuchapishwa — mapitio ya nusu mwaka na taarifa ya mwisho wa mwaka. Hivyo basi, ni taarifa sita tu za bajeti ndizo zilizokuwa zimechapishwa hadi kufikia mwisho wa nusu-muhula. Taarifa zilizokuwa zimechapishwa ni taarifa kabla ya bajeti; muhtsari wa mapendekezo ya bajeti; bajeti iliyopitishwa; bajeti ya wananchi; taarifa za kila mwaka juu ya mapato yaliyokusanywa, matumizi na madeni; na taarifa za wakaguzi.

Taarifa nyingine muhimu kutolewa chini ya azimio hili hazikutolewa, ikiwa ni pamoja na taarifa za misamaha ya kodi, taarifa za kamati za ukaguzi za bunge, na uchapishaji wa taarifa hizi za budget katika mfumo unaowezesha kusomwa na kompyuta/mashine.

Mwishoni: Kiasi kidogo

Hadi kufikia mwisho wa mzunguko wa utekelezaji (yaani 30 Juni 2016), serikali ilikuwa imechapisha saba kati ya taarifa kuu nane za bajeti, ingawa si zote ziliwekwa wazi kwa umma. Taarifa kuu saba za bajeti zilizokuwa zimechapishwa ni (1) taarifa kabla ya bajeti; (2) muhtsari wa mapendekezo ya bajeti; (3) bajeti iliyopitishwa; (4) bajeti ya wananchi; (5) taarifa za kila mwaka juu ya mapato yaliyokusanywa, matumizi na madeni; (6) mapitio ya nusu-mwaka; na (7) taarifa za wakaguzi. Taarifa ya mwisho wa mwaka (utekelezaji bajeti) ilikuwa ikiandaliwa lakini haikuchapishwa² hadi tulipokuwa tukiandika taarifa hii.

Taarifa ya kujitathmini ya serikali ya 30 Juni 2016 inaeleza kuwa taarifa za misamaha ya kodi na kamati za ukaguzi za bunge ziliwekwa mtandaoni—kwenye tovuti za Wizara ya Fedha na Bunge. Hata hivyo, ukaguzi uliofanywa na mtafiti wa IRM ulionyesha kuwa baadhi ya taarifa hizi hazikukamilika, zimepitwa na wakati, au hazikuchapishwa kabisa. Misamaha ya kodi na nyaraka muhimu za kodi zilipaswa kutolewa kila mwezi, lakini ni taarifa mbili tu kati ya nne za robo-mwaka zilichapishwa kwa mwaka 2015.³ Taarifa za kamati za ukaguzi za bunge hazikukamilika katika mzunguko wa utekelezaji wa mpango kazi wa pili.

JE, AZIMIO LILIFUNGUA SERIKALI?

Upatikanaji taarifa: Kiasi kidogo

Uwajibikaji kwa wananchi: Kiasi kidogo

Azimio lililenga kuboresha uwazi katika masuala ya fedha kwa kuweka wazi taarifa kuu nane za bajeti, misahama ya kodi, na taarifa za kamati za ukaguzi za bunge. Katika kipindi cha azimio mnamo mwaka 2015, serikali ya Tanzania ilitoa sita kati ya nyaraka nane za bajeti zilizokuwa zitolewe mwaka 2014. Hata hivyo, mapitio ya nusu-mwaka na taarifa ya mwisho wa mwaka hazikutolewa.

Kwa mujibu wa Open Budget Survey, hadi kufikia Aprili 2016 Tanzania ilikuwa imerudi nyuma kwa hatua tangu ilipopimwa kwa kipindi kama hicho mwaka 2015, ikiweka wazi nyaraka tano tu kati ya nane za bajeti. Taarifa ambazo huko nyuma zikipatikana za kila mwaka (mapato, matumizi na madeni) zilichapishwa kwa matumizi ya ndani ya serikali tu. Hadi kufikia Septemba 2016, taarifa za kila mwaka, mwisho wa mwaka, na nusu-mwaka hazikuwekwa wazi ili kufikiwa na umma,⁴ wakati ambapo taarifa kabla ya bajeti; muhtsari wa mapendekezo ya bajeti; bajeti iliyopitishwa; bajeti ya wananchi; na taarifa za ukaguzi ziliendelea kuwa wazi na kufikiwa.

Ahadi ya serikali ya kuchapisha takwimu nyingi za bajeti, sambamba na taarifa za kodi na ukaguzi, zingeweza kubadili kwa kiasi kikubwa uendeshaji na nidhamu ya fedha nchini Tanzania. Juu ya hayo, taarifa mpya zingeweza kuweka msingi kwa miundo thabiti ijayo ya kuhakikisha takwimu za bajeti zinachapishwa.

Wakati wa kipindi cha azimio, serikali ilianza kutoa nyaraka za misamaha ya kodi ambazo huko nyuma hazikuwepo. Taarifa ya kujitathmini ya serikali ya 30 Juni 2016 inaeleza kuwa taarifa za misamaha ya kodi na kamati za ukaguzi za bunge ziliwekwa mtandaoni—kwenye tovuti za Wizara ya Fedha na Bunge. Hata hivyo, uchunguzi wa mtafiti wa IRM ulionyesha taarifa za robo-mwaka mbili za misamaha ya kodi kwa vipindi vya Aprili–Juni and Julai–Septemba 2015 zilichapishwa mwishoni kabisa wa tarehe ya mwisho ya tathmini ya taarifa hii (30 Juni 2016), ikimaanisha kuwa taarifa mbili za robo mwaka ziko nyuma na baadhi ya taarifa za mwaka wa fedha 2014–2015 hazikuchapishwa kabisa.⁵ Tovuti ya Bunge (www.bunge.go.tz) haikuonyesha taarifa zozote za kamati za ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2014–15 na 2015–16.

Wadau wa asasi za kiraia⁶ waliona ya kuwa serikali imekuwa ikichapisha taarifa kuu nane za bajeti kabla ya muda wa utekezaji wa azimio kupita hivyo kujumuishwa kwake hakukuwa na athari yoyote katika kubadili utendaji wa serikali. Hata hivyo, kuchapisha taarifa za misamaha ya kodi na zile za kamati za ukaguzi za bunge ingekuwa na atahri kubwa ya kuongeza imani ya Wananchi kwa serikali kwani ingewapa Wananchi taarifa za kina juu ya bajeti na matumizi ya serikali ambazo huko nyuma hazikuwa zikiwekwa wazi. Pia, kuwea wazi taarifa kuu tatu za bajeti zilizokuwa zimesalia kuchapishwa kati ya nane zinazoandaliwa na serikali ingekuza uwazi.

KIPI KILICHOSOGEZWA MBELE?

Rasimu ya tatu ya mpango kazi wa OGP wa Tanzania⁷ inajumuisha azimio la kuchapisha takwimu za bajeti mtandaoni kupitia hatua zinazofanana na zile za mpango kazi wa pili wa OGP. Badiliko pekee likiwa kwamba serikali sasa imedhamiria kuchapisha taarifa ya misamaha ya kodi kila robo-mwaka badala ya kila mwezi. Pia serikali inatarajia kutoa waraka kwa mamlaka za serikali za mitaa, shule, na vituo vya afya kuhakikisha kuwa maelezo ya kina ya bajeti na matumizi zinapatikana kwa mkazi akiomba na kubandikwa kwenye mbao za matangazo.

¹ Open Budget Survey, 30 April 2016, <http://www.internationalbudget.org/budget-work-by-country/findgroup/group-data/?country=tz>.

² Mahojiano na afisa wa serikali ambaye hakutaka kutajwa, 25 Agosti 2016, Dar es Salaam.

³ Taswira ya tovuti ya Wizara ya Fedha ilivyoonekana, mnamo 20 Oktoba 2016. Inapatikana http://www.mof.go.tz/index.php?option=com_content&view=category&id=80&Itemid=999.

⁴ Open Budget Survey, 30 April 2016, <http://www.internationalbudget.org/budget-work-by-country/findgroup/group-data/?country=tz>.

⁵ Taswira ya tovuti ya Wizara ya Fedha ilivyoonekana, mnamo 20 Oktoba 2016. Inapatikana http://www.mof.go.tz/index.php?option=com_content&view=category&id=80&Itemid=999.

⁶ Mahojiano kwa njia ya simu na mdau wa asasi za kiraia, 13 Oktoba 2016, Dar es Salaam.

⁷ Tanzania Open Government Partnership (OGP) Third National Action Plan 2016-18, http://www.twaweza.org/uploads/files/FINAL%20OGP%20ACTION%20PLAN%20III%2030_8_2016.pdf

3.4 | UWAZI KATIKA MASUALA YA ARDHI

Maelezo kamili ya azimio:

Kuhakikisha kuwa kuna upatikanaji wa mipango ya matumizi ya ardhi, umiliki na maeneo yaliyotengwa kwa uwekezaji mkubwa mtandaoni kwa matumizi ya umma hadi itakapofika Juni 2016.

Hii inajumuisha mambo yafuatayo:

- (i) Kuchapisha taarifa za maeneo yaliyotengwa kwa uwekezaji mkubwa wa kilimo (ukulima na ufugaji)
- (ii) Kuchapisha mipango yote ya matumizi ya ardhi na kufanya yawafikie wananchi kuanzia ngazi ya taifa hadi ya msingi.
- (iii) Kuweka mtandaoni kanzi ya takwimu za umiliki ardhi ambazo ni rahisi kuzitafuta.

Taasisi kiongozi: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (MLHSD)

Taasisi saidizi: Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Kituo cha Uwekezaji (TIC), AzaKi na asasi za sekta binafsi ambazo hazikutajwa

Tarehe ya kuanza: Haikutajwa

Tarehe ya mwisho: 30 Juni 2016

MAPITIO YA AZIMIO	UMAHUSUSI				UHUSIANO NA TUNU ZA OGP (kama ilivyoandikwa)				ATHARI TARAJALI				UTEKELEZAJI		NUSU-MUHULA MWISHONI		JE, ILIIFUNGUA SERIKALI?				
	Hakuna	Mdogo	Wastani	Uko juu	Upatikanaji taarifa	Ushiriki wa wananchi	Uwajibikaji kwa umma	Teknolojia & Ubunifu kwa ajili ya Uwazi & Uwajibikaji	Hakuna	Ndogo	Wastani	Mabadiliko makubwa	Haujaanza	Kiasi kidogo	Kiasi kikubwa	Umekamilika	Iliharibika	Haikubadilika	Kiasi kidogo	Kiasi kikubwa	Imejipambanua
3.4. Kwa ujumla			X		X		X			X			X						X		

LENGO LA AZIMIO:

Azimio limelenga kuhakikisha usimamizi wa haki na usawa wa rasilimali ardhi kwa kuchapisha mipango ya matumizi ya ardhi, taarifa za umiliki, na maeneo yaliyotengwa. Migogoro ya matumizi ya ardhi ni changamoto kubwa nchini Tanzania na ni chanzo cha mapigano ya mara kwa mara kati ya wakulima na jamii za wafugaji, na pia kati ya jamii vijijini na wawekezaji.¹ Serikali iliahidi kuchapisha maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji mkubwa katika kilimo (mf., kilimo na ufugaji) na kuweka kanzi mtandaoni inayoweza kutafuta kwa urahisi taarifa kuhusu umiliki ardhi nchini Tanzania. Azimio hili linaweza kuchangia katika kuleta ufumbuzi wa migogoro ya ardhi iliyosambaa nchi nzima kati ya wakulima na jamii za wafugaji ambazo ni majirani. Migogoro karibu yote bado inaendelea kuwepo na haijapatiwa ufumbuzi. Jamii pia zina mgongano na wawekezaji, ambapo mara kwa mara wawekezaji wameshutumiwa kupora ardhi.²

HALI ILIVYO

Nusu-muhula: Kiasi kidogo

Kufikia nusu-muhula, azimio hili lilikuwa limekamilika kwa kiasi kidogo huku upimaji wa awali wa ardhi ukiwa umefanyika kwenye mkoa mmoja tu, Morogoro. Hatua za awali za kuanzisha kanzi mtandaoni zimekuwa zikiendelea, ingawa hakuna takwimu iliyokuwa imechapishwa mtandaoni kuhusiana na mipango ya matumizi ya ardhi na/au maeneo yaliyotengwa.

Mwishoni: Kiasi kidogo

Taarifa ya kujitathmini ya serikali (hadi kufikia 30 Juni 2016) inaeleza kuwa orodha ya maeneo 348 yaliyotengwa kwa uwekezaji mkubwa wa kilimo huko kanda ya Mashariki ya Tanzania yametambuliwa na kuthibitishwa, lakini takwimu hizi hazijawekwa mtandaoni. Katika mahojiano yaliyofanyika kwa njia ya simu na mtafiti wa IRM³, afisa wa serikali alithibitisha idadi hiyo ya maeneo yaliyotengwa na upimaji uliofanyika kwenye vijiji mkoani Morogoro—15 wilayani Morogoro, 25 wilayani Kilosa, na 25 wilayani Mvomero—upimaji ambao utapelekea kuandaa mipango ya matumizi ardhi. Taarifa hizi zilidaiwa kuwekwa kwenye tovuti ya wizara ya ardhi (MLHSD). Hata hivyo, mtafiti wa IRM hakukuta mipango yoyote ya matumizi ya ardhi iliyochapishwa kwenye tovuti hiyo ya wizara.

Zaidi, katika mahojiano hayohayo, mtafiti wa IRM alithibitishiwa kuwa mkandarasi wa kutengeneza kanzi ya mtandaoni ya masuala ya ardhi (ILMIS) ameshafahamika, sampuli ya awali ilishazinduliwa, na hatua inayofuata ni kwa mkandarasi kuendelea kuiunda kazi hiyo (ILMIS). Ili kukamilisha azimio hili, serikali lazima imalizie kutengeneza kanzi hiyo na ipatikane mtandaoni, ichapishe mtandaoni mipango ya matumizi ardhi, na kuweka wazi maeneo yote yaliyotengwa kwa ajili ya matumizi ya biashara na uwekezaji mkubwa wa kilimo.

JE, AZIMIO LILIIFUNGUA SERIKALI?

Upatikanaji taarifa: Kiasi kidogo

Uwajibikaji kwa wananchi: Haikubadilika

Azimio limelenga kuweka wazi na kuchapisha mipango ya matumizi ya ardhi, taarifa za umiliki, na maeneo yaliyotengwa. Ardhi nchini Tanzania ni mali ya serikali, huku Rais akiwa ndio mhifadhi kwa niaba ya raia. Watu binafsi wanaweza kumiliki ardhi kupitia hati zinazotolewa na serikali. Tatizo limekuwa kukosekana kwa mipango ya matumizi ya ardhi na kwamba ardhi imekuwa ikiuzwa kwa bei ya mara moja tu bila kuzingatia kuwa ardhi inaongezeka thamani kadiri muda unavyoenda.⁴ Zaidi, upimaji ardhi ukigharamiwa na mtu mmoja mmoja ni gharama kubwa, na unatofautiana mno bei-kwa-kila-ekari moja. Mara nyingi vijiji vinakuwa na hati za umiliki ardhi kimila (CCROs) ambazo haziwezi kutumika kama dhamana kwenye mabenki. Kwahiyo, azimio hili, ambalo pamoja na mambo mengine linadhamiria kuchapisha mipango ya matumizi ya ardhi (ndani na nje ya mtandao katika ngazi ya jamii), ni muhimu sana katika kushughulikia migogoro ya ardhi na kuboresha usimamizi wa masuala ya ardhi nchini Tanzania.⁵

Hatua zilizochukuliwa na serikali, kama vile kuyatambua maeneo yaliyotengwa na kufanya upimaji, zinaonyesha mageuzi kwa kiasi Fulani katika utendaji kazi wa serikali. Ikizingatiwa kuwa kuna ufinyu wa upenyaji wa intaneti nchini Tanzania, kuchapisha taarifa za ardhi mtandaoni si njia bora ya kufikia hadhira pana. Hata hivyo, serikali haikukuza ubora wa taarifa na takwimu zilizochapishwa kuhusiana na masuala ya ardhi. Taarifa zilizopo sasa zinajumuisha orodha ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya matumizi ya uwekezaji mkubwa katika kilimo. Taarifa hizi hazikuwa zikipatikana kwa urahisi hapo awali, na ingawa takwimu za ziada juu ya ukubwa na matumizi ya uwekezaji kwa kila eneo tengwa haziko wazi, ahadi ya kuwa na takwimu za ardhi za aina hii yaweza kuwa na matokeo chanya wakati ambapo seti za takwimu zaidi zikitolewa hapo siku za usoni. Mtafiti wa IRM na wadau wa AzaKi waliohojiwa⁶ wanaamini kuwa kukamilika kwa azimio hili kutabadilisha namna mamlaka serikalini, hasa zilizopo maeneo ya vijijini, zitakavyofanya kazi na kuleta utendaji bora wa usimamizi wa ardhi nchini Tanzania. Ingawa kazi hii bado haijakamilika, asasi za kiraia zilikuwa na maoni kuwa kukamilika kwa azimio hili kutabadilisha kwa kiasi

kikubwa namna serikali inavyopanga, kugawa, na kwa ujumla kusimamia ardhi kwa uwazi zaidi, kuwa jibu kwa karibu migogoro yote iliyopo ya ardhi.

KIPI KIMESOGZWA MBELE?

Azimio hili limesogezwa mbele kwa kujumuishwa kwenye rasimu ya mpango kazi wa tatu wa OGP (2016/17–2017/18). Hatua zinazofuata kwa azimio hili ni pamoja na, ingawa si zote, kuchapisha mtandaoni maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji mkubwa katika kilimo na kuchapisha mipango ya matumizi ardhi kwenye kanzi inayoendelea kuundwa ya ILMIS.

¹IRM Progress Report.

²Songa wa Songa, "SPECIAL REPORT: Land grabbing in Tanzania: The truth, fallacies and fights-part 1," The Citizen, 24 March 2015, <http://bit.ly/1NQuGc8>.

³Mahojiano kwa njia ya simu na afisa wa serikali ambaye hakutaka kutajwa, 22 Septemba 2016, Dar es Salaam.

⁴Kizito Makoye, "Complex land rights feed 'grabbing' complaints in Tanzania," Reuters, 17 April 2014, <http://news.trust.org/item/20140417110316-z13bv/?source=spotlight>.

⁵Deodatus Mfugale, "Tanzania: Land Use Plans May Solve Conflicts, Attract Investment," Daily News, 16 December 2014, <http://allafrica.com/stories/201412160029.html>.

⁶Mahojiano ya ana-kwa-ana na mdau wa asasi za kiraia ambaye hakutaka kutajwa, 30 Septemba 2016, Dar es Salaam.

3.5 | UWAZI KATIKA SEKTA YA UZIDUAJI

Maelezo kamili ya azimio:

Tanzania itekeleze maazimio yake ya EITI hadi kufikia Juni, 2015

Hii inajumuisha mambo yafuatayo:

(i) Kuchapisha mikataba ya uendelezaji wa madini (MDAs) na Kandarasi za Kugawana Faida (PSCs) ya tangu 2014 na kuendelea itakapofika Juni, 2015;

(ii) Kunakili sera ya serikali kuhusu utoaji wa taarifa za kandarasi au mikataba iliyosainiwa kabla ya Juni, 2015; na

(iii) Kuchapisha maeneo yaliyotengwa kwa uchimbaji madini hadi kufikia Desemba, 2014.

Taasisi kiongozi: Wizara ya Nishati na Madini (MEM)

Taasisi saidizi: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG)

Tarehe ya kuanza: Haikutajwa

Tarehe ya mwisho: 31 Desemba 2015

MAPITIO YA AZIMIO	UMAHSUSI				UHUSIANO NA TUNU ZA OGP (kama ilivyoandikwa)				ATHARI TARAJALI				UTEKELEZAJI		NUSU-MUHULA MWISHONI		JE, ILIIFUNGUA SERIKALI?				
	Hakuna	Mdogo	Wastani	Uko juu	Upatikanaji taarifa	Ushiriki wa wananchi	Uwajibikaji kwa umma	Teknolojia & Ubunifu kwa ajili ya Uwazi & Uwajibikaji	Hakuna	Ndoto	Wastani	Mabadiliko makubwa	Haujaanza	Kiasi kidogo	Kiasi kikubwa	Umekamilika	Iliharibika	Haikubadilika	Kiasi kidogo	Kiasi kikubwa	Imejipambanua
3.5. Kwa ujumla				X	X	X				X		X							X		

LENGO LA AZIMIO:

Azimio linalenga kukidhi masharti ya Jukwaa kimataifa la Uwazi katika sekta ya Uzidujaji - *Extractive Industries Transparency Initiative* (EITI) kwa kuchapisha mtandaoni nyaraka muhimu kadhaa ambazo zingeboresha uwazi katika masuala ya Uzidujaji (EI) nchini Tanzania. Hadi wakati taarifa hii inaandikwa, Tanzania ilikuwa imekidhi masharti ya EITI, na shughuli zilizopendekezwa kufanywa ndani ya azimio hili zilikuwa ni chachu zaidi ya kukuza uwazi katika sekta ya uzidujaji. Pia, azimio hili linadhamiria kurudisha imani ya Wananchi kwa kuweka lazima ya uwazi wa mikataba ya uendelezaji wa madini (MDAs) na Mikataba ya Kugawana Faida kwa sekta ya gesi (PSCs) iliyosainiwa kabla na baada ya sheria ya Uwazi na Uwajibikaji kwenye sekta ya Uzidujaji - *Tanzania Extractive Industries Transparency and Accountability (TEITA) Act* kuanza kufanya kazi mnamo 16 Oktoba 2016.¹ Kukamilika kwa utekelezaji wa azimio hili kunaweza kuupa fursa umma wa kufikia taaifa juu ya mapato yatonakanayo na madini, mafuta na gesi asilia nchini Tanzania.

HALI ILIVYO

Nusu-muhula: Haujaanza

Hadi kufikia nusu-muhula, serikali ilikuwa bado haijaanza kutekeleza shughuli yoyote inayotokana na azimio hili. Nchi ya Tanzania ilisimamishwa uanachama wa EITI sababu ya kushindwa kuchapisha taarifa za EITI zilizohitajika kupelekwa kabla ya tarehe 30 Juni 2015.

Mwishoni: Kiasi kidogo

Hatua muhimu zilizoweka misingi ya uwazi zaidi katika sekta ya uziduaji nchini Tanzania zimekuwa zikiendelea.

Mnamo Julai 2015 Bunge lilipitisha sheria tatu: Sheria ya Petroli ya 2015, Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji kwenye sekta ya Uziduaji ya 2015 (TEITA), na Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Gesi na Mafuta. Sheria hizo zilihuisha na kuongeza wigo wa sheria zilizokuwepo kwa upande wa sekta ya gesi na mafuta. Sheria ya Petroli inaweka viwango vya kodi kwa wenye leseni na wakandarasi katika sekta ya uziduaji. Sheria ya TEITA inashurutisha miliki, mikataba, na leseni kuwekwa wazi na kufikiwa na umma. Tanzania inaungana na orodha ya nchi chache ambazo tayari zina sheria kuhusiana na masuala ya EITI pekee, nah ii ni muhimu kwani makampuni yote katika sekta ya uziduaji yaliyopo nchini lazima yaweke wazi akina nani hasa ndio wamiliki w makampuni hayo. Tawi la EITI Tanzania (TEITI) pia limechapisha taarifa ya awali iliyopitia muundo wa kisheria na kitaasisi kuhusu uwazi wa wamiliki halisi, taarifa hiyo inapatikana mtandaoni tangu 26 Machi 2016. Juhudi zote hizi zinalenga katika kuongeza uwazi kwa sekta ya uziduaji nchini Tanzania.

Licha ya hatua hii iliyopigwa na mabadiliko yanayoletwa na sheria hizo, shughuli hususan kwa azimio hili, kama vile kuchapisha MDAs na PSCs, zimetokelezwa kwa kiasi kidogo. Uwekaji wazi na uchapishaji wa mikataba hiyo ni muhimu kwa msimamo wa nchi katika jamii ya EITI na katika kuifungua zaidi sekta ya uziduaji nchini Tanzania.

Taarifa ya kujitathmini ya serikali (hadi kufikia 30 Juni 2016), inadai kuwa nigodi mikubwa 217 kati ya 423 ilikuwa imeshasajiliwa kwenye kanzi ya miamala ya madini mtandaoni (OMCTP), ambayo inatumwa kama hifadhi ya pango zote za madini,² maombi ya leseni au vibali, ramani za jiolojia, na picha za satelaiti. Mtafiti wa IRM alithibitisha tathmini hiyo ya serikali alipopitia kanzi hiyo ya OMCTP.³ Watendaji wa asasi za kiraia⁴ wanaeleza kuwa tovuti kuu hiyo ya madini ni jukwaa la kuwawezesha wateja kusajili maombi, kukagua leseni zao, kutuma taarifa za ufanisi wa kazi zao, na kuwawezesha malipo ya leseni na mirabaha kwa njia ya kielektroniki.

Ili kukamilisha azimio hili kwa utimilifu, serikali inahitaji kuchapisha sera ya namna mikataba imekuwa ikiwekwa wazi hapo awali, mbali na kuchapisha mikataba yote MDAs na PSCs iliyosainiwa tangu mwaka 2014 na kuendelea kwa kuiweka mtandaoni na nje ya mtandao. Kupitia kanzi ya OMCTP, serikali imeanza kuchapisha taarifa zinazotakiwa na zenye umuhimu kwa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uchimbaji mkubwa wa madini, lakini wadau walikuwa na maoni kuwa taarifa zaidi zinatakiwa kuwekwa wazi, ikiwa ni pamoja na mifumo nje ya mtandao na kwa lugha ya Kiswahili.⁵

JE, AZIMIO LILIFUNGUA SERIKALI?

Upatikanaji taarifa: Kiasi kidogo

Uwajibikaji kwa wananchi: Haikubadilika

Tanzania ni mwanachama wa EITI, kitu kinachoonyesha dhamira ya nchi kufanya takwimu na mapato katika tasnia ya uziduaji kuwa wazi zaidi kwa kufikiwa na kuhojiwa na Wananchi. Kwa sasa nchi imekidhi masharti ya EITI, ingawa ilikosea kidogo kwa tathmini ya kipindi cha nusu-muhula. Azimio hili ni hatua ya mwelekeo sahihi kisera ili kuhakikisha usimamizi bora na wazi wa tasnia ya uziduaji. Huko nyuma, vyombo vya habari viliripoti juu ya kesi za rushwa ikijumuisha mikataba katika sekta ya madini baina ya serikali na makampuni ya uziduaji [kwa mikataba iliyosainiwa kabla ya 2014], huku rushwa na ulafi vikiishawishi kusainiwa kwa siri mikataba ya MDAs na PSCs. Pamoja na hayo, nakala ya mwisho ya sheria ya TEITA (Kifungu cha 27) kinaruhusu kuweka wazi mikataba yote

hata ile iliyosainiwa kabla ya sheria kuanza kutumika. Kwa mujibu wa mdau mmoja wa asasi za kiraia,⁶ kanzi ya OMCTP inasiadia kupambana na rushwa, inaongeza ufanisi kwa upande wa watumishi wizarani, na pia kuzisaidia taasisi za uangalizi kupata takwimu zitakazowawezesha kufuatilia mapato, usimamiaji, na uwazi katika sekta ndogo ya madini.

Hata hivyo, mdau huyo⁷ alionelea ya kuwa ili kupiga hatua kubwa na kuifungua sekta ya uziduaji kwa umma kuweza kuhoji bila vikwazo vyovyote, budi serikali isimamie kwa ukamilifu utekelezaji wa vifungu vilivyomo kwenye sheria ya TEITA. Hii ni pamoja na kuhakikisha mikataba na kandarasi zilizosainiwa kama sheria inavyotaka. Mdau mmoja wa asasi za kiraia alisema kuwa juu ya kufahamu wanaomiliki leseni, wananchi wana hamu zaidi ya kupata taarifa zinazoonyesha ni kwa namna gani nchi inafaidika kutokana na mikataba hii.⁸

Utekelezaji kamilifu wa sheria ya TEITA utasaidia kuweka wazi taarifa ambazo hapo awali zilikuwa ni siri ya serikali kwa upande mmoja na makampuni ya madini, mafuata na gesi kwa upande mwingine. Mtafiti wa IRM ana imani kuwa kwa kasi inayoendelea ya serikali kuu kusimamia nidhamu ya fedha kwa wizara, idara na wakala wake (MDAs), sasa mazingira ni pevu kwa kuifungua serikali zaidi hususan sekta ya uziduaji.

KIPI KIMESOGEZWA MBELE?

Azimio hili pia limesogezwa na kujumuishwa kwenye rasimu ya tatu ya mpango kazi wa OGP. Hatua zinazotakiwa kufuata kwa azimio hili ni pamoja na, kuchapisha mtandaoni maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uchimbaji mkubwa wa madini na kuweka mikataba na kandarasi kwenye tovuti ya wizara ya Nishati na Madini.

¹The Tanzania Extractive Industries (Transparency and Accountability) Act, No. 23 of 2015. Imepakuliwa tarehe 16 Oktoba 2016 at <http://www.teiti.or.tz/wp-content/uploads/2016/02/Date-Commencement-of-TEITA-Act2015.pdf>.

²Pango la mgodi wa madini ni kibali, madai, leseni, au pango ambalo linaweza kutolewa na msajili mgodi au waziri wa nishati na madini.

³<http://portal.mem.go.tz/map/>.

⁴Mahojiano na mdau wa asasi za kiraia, 24 Oktoba 2016, Dar es Salaam.

⁵Mahojiano na mtaalamu wa EITI kutoka AzaKi, 24 Oktoba 2016, Dar es Salaam.

⁶Mahojiano kwa njia ya simu na mdau wa asasi za kiraia, 13 Oktoba 2016, Dar es Salaam.

⁷Ibid.


⁸Ibid.

MAELEZO YA METHODOLOJIA

Maazimio yanachambuliwa kwa namna yalivyoandikwa, ingawa kwa kifupi, kwenye mpango kazi wa pili wa OGP nchini Tanzania (2014–2016). Taarifa hii ya tathmini ni matokeo ya mchanganyiko wa mbinu za kukusanya takwimu, pamoja na mapitio ya azimio kwa rasilimali za mtandaoni; mapitio ya sheria, kanuni na nyaraka za serikali yaliyofanywa na mtafiti mwenyewe; na mapitio ya taarifa ya kujitathmini ya serikali iliyoonyesha utekelezaji mwishoni mwa mzunguko wa kipindi cha miaka miwili.

Mtafiti wa IRM pia alipitia maazimio kwa vipindi vya nusu-muhula na mwishoni na kufanya mahojiano na maafisa walioteuliwa serikalini na wadau wa asasi za kiraia ili kutathmini utekelezaji ulivyokuwa mwishoni.

Maafisa wa serikali tisa toka wizara, idara, na wakala walihojiwa wakati wa tathmini ya mwisho. Hawa walikuwa kutoka Ofisi ya Rais-Kitengo cha Kuratibu Utawala Bora (PO-GGCU), wizara ya Fedha, OR-TAMISEMI, wizara ya Katiba na Sheria (MoCLA), wizara ya Afya, wizara ya Elimu na Sayansi, TEITI, wakala wa Serikali Mtandao, Idara ya Habari (MAELEZO). Pia, mtafiti aliwahoji wadau watatu wa vyombo vya habari kutoka *Tanzania Media Fund*; *Nipashe*, gazeti la kila siku; na *Raia Mwema*, ambalo ni gazeti la kila wiki kwa lugha ya Kiswahili. Mtafiti huyo wa IRM pia aliwahoji wadau sita wa asasi za kiraia kutoka Hakiardhi, ForDIA, Twaweza, Tanzania Information Bureau, Kisarawe Women Group, na Ubunifu Associates.



Ngunga Greyson Tepani ni Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Association of Non-Governmental Organisations (TANGO). Ana shahada ya Uzamili kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Open
Government
Partnership

INDEPENDENT
REPORTING MECHANISM

Mpango wa Utendaji Kazi wa Serikali kwa Uwazi (OGP) una lengo la kupata maazimio mahususi kutoka katika serikali mbalimbali yatakayohimiza uwazi, kuwezesha wananchi, kupambana na rushwa, na kutumia teknolojia mpya ili kuboresha utawala bora. Mfumo wa Tathmini wa Taarifa za OGP (IRM) unahakiki uundaji na utekelezaji wa mipango kazi ya nchi mbalimbali ili kukuza majadiliano miongoni mwa wadau na kukuza uwajibikaji.



Independent Reporting Mechanism
Open Government Partnership
c/o OpenGovHub
1110 Vermont Ave NW Suite 500
Washington, DC 20005

